HOTUBA YA MENEJA MPANGO WA TAIFA WA CHANJO WIZARA YA AFYA DR. MARY KITAMBI KWENYE SEMINA YA WAANDISHI WA HABARI KUHUSU KAMPENI YA UGONJWA WA PEPOPUNDA TAREHE 21/8/2009. KATIKA UKUMBI WA MPANGO WA TAIFA WA CHANJO.

Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa
Wawakilishi wa Vyombo vya Habari,
Wawakilishi wa Wizara ya Afya na Wizara zingine,
Washiriki, Mabibi na Mabwana,

Napenda kutoa shukurani zangu nyingi kwa kupewa nafasi ya kufungua Semina hii muhimu. Aidha kwa niaba ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, naomba nichukue nafasi hii niwashukuru kwa kuitikia wito wa kuhudhuria semina hii. Ninaelewa majukumu yenu ni mengi na muhimu katika kuihamasisha jamii.

Aidha nachukua nafasi hii kuwakaribisha katika ukumbi huu ili tuweze kukumbushana tena kuhusu ugonjwa wa Pepopunda, chanjo inayotolewa kuzuia ugonjwa huu na kampeni za chanjo ya Pepopunda zinazoendelea hapa nchini katika baadhi ya mikoa na wilaya zilizo ainishwa ambazo zimeonekana kuwa na tatizo la ugonjwa wa pepopunda kwa watoto wachanga. Wilaya / Halimashauri hizo ni:- Ngara, Kibondo, Bariadi, Kahama, Bukombe, Meatu, Simanjiro, Hanang, Kiteto, Tarime, Rorya, Bunda, Mpanda Vijijini na Halimashauri ya wilaya ya Mpanda.

Kampeni hii inaendeshwa katika awamu tatu:-

1. awamu ya kwanza mwezi mei tarehe 23 na 24, 2009
2. awamu ya pili mwezi juni tarehe 26 na 27, 2009

3. Awamu ya tatu ya kampeni hii itakuwa mwezi January ,2010.

Ndugu washiriki,
Wizara ya afya na Ustawi wa Jamii inakawaida ya kuendesha Semina za Waandishi wa habari kabla ya kuanzisha au kuendesha zoezi lolote au kampeni yeyote, na hii husaidia sana kufanikisha malengo yetu kwa kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu jambo litakalotendeka na huleta mwitikio mkubwa wa Jamii.

Kwa bahati mbaya safari hii hatukuweza kuendesha semina kutokana na mwingiliano wa shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa chanjo mpya ya Pentavalent na utekelezaji wa mafunzo ya mkakati wauinuaji chanjo nchini "RED approach"na mengine mengi. Hata hivyo tulishawasiliana nanyi kwa kuwaletea ujumbe kuhusu kampeni ya chanjo Pepopunda kwa wanawake wenye umri wa kuzaa miaka 15 hadi 49 inayoendelea nchini, na ujumbe huo mmeisha urusha kupitia vyombo vyenu mbalimbali vya habari ili kuelimisha jamii.

Pamoja na kuchelewa, leo tumeona tuwaite ili tuungane nanyi kuhusu mwendelezo wa kampeni ya chanjo ya Pepopunda kwa awamu ya tatu ijayo, chanjo hii itatolewa mwezi januari mwaka 2010. Hivyo kama nilivyosema awali, madhumuni yetu ya kuwaita ni kutaka:

1. Kuwaelimisha jinsi ugojwa wa Pepopunda unavyoamukizwa, dalili, matibabu, chanjo yake na madhara yatokanayo na ugojwa huu.

2. Walengwa wa chanjo hii hutolewa kwa watoto na wanawake walio katika umri wa kuzaa, ratiba ya chanjo kwa mtoto na mwanamke walio katika umri wa kuzaa.

3. Kuwapa matokeo ya awali ya kwa awamu mbili za kampeni ya chanjo ya Pepopunda zilizopita.

Ndugu washiriki,
Ugonjwa wa pepopunda ni ugonjwa hatari unaoambukizwa na viini vya bakteria viitwavyo 'clostridium tetani. Viini hivi huingia mwilini kupitia kidonda au jeraha. Kwa watoto wachanga toka wanapozaliwa hadi kufikia umri wa siku 28, Viini hivi huingia mwilini kupitia kwenye kitovu kilichokatwa

kwa kutumia kitu kichafu kama vile wembe, mabua au usinge na kuwekwa vitu vichafu kama vile kinyesi cha ng'ombe au vumbi la kizingiti n.k.
Pepopunda ni ugonjwa unaosababisha vifo vya watoto wachanga katika nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania. Asilimia 14 ya vifo vyote vya watoto wachanga ulimwenguni kote hutokana na ugonjwa wa Pepopunda. Hata hivyo ni vigumu kupima ukubwa halisi wa tatizo kwani vifo vingi hutokea nyumbani kabla ya mtoto hajafikisha wiki mbili na mara nyingi taarifa ya kuzaliwa kwa mtoto wala kifo haitolewi. Ugonjwa halisi wa pepopunda kwa watoto wachanga hutokea endapo mama atajifungua katika mazingira yasiyo safi na salama.

Ndugu washiriki,
Chanjo ya Pepopunda
Chanjo ya Pepopunda ilianza kutumika kuanzia mpango wa chanjo ulipoanzishwa hapa nchini. Tanzania ni moja ya nchi ambazo zina utaratibu madhubuti wa kutoa chanjo kwa watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja na wanawake wenye umri wa kuzaa miaka 15 hadi 49. Chanjo ya pepopunda kwa watoto hutolewa kuanzia mtoto anapokamilisha wiki nne hivyo, ili kumkinga mtoto mchanga na ugonjwa huu, njia pekee ni kumchanja mama kabla ya ujauzito.

WALENGWA
Walengwa wa chanjo ya pepopunda ni Wanawake wenye umri wa uwezo wa kuzaa miaka 15 hadi 49 na watoto chini ya umri wa mwaka mmoja. Kufuatana na Sera ya Tanzania Bara dozi ya kwanza hutolewa kwa mtoto mwenye umri wa wiki nne, ya pili umri wa wiki nane na ya tatu umri wa wiki kumi na mbili.

Ndugu washiriki,
Naamini kuwa semina hii itatoa nafasi nzuri ya kuwaelimisha zaidi kuhusu ugonjwa wa pepopunda, chanjo na Kampeni za pepopunda zilizofanyika na itakayoendeshwa mwakani. ili muendelee kuielemisha na kuihamasisha jamii kuhusu ugonjwa huu hatari.

Mwisho, napenda niwashukuru tena kwa kukubali mwaliko wetu, na niwatakie majadiliano mema yatakayo iwezesha Jamii kuufahamu zaidi

ugonjwa wa pepopunda na walengwa wa chanjo hii ili kupunguza madhara na adhari za ugonjwa huu hapa nchini.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.